

# Milenia 2015

## Wanawake Washiriki wa Maendeleo kwa ajili ya Changamoto za Dunia

---

### Milenia 2015, Majukumu na Dhima Yake

Eleonora Barbieri Masini

Januari 2010

---

#### Utangulizi:

Msingi muhimu Milenia 2015 kama jina lake linavyoonesha ni mkazo katika kutambua majukumu ya wanawake kwenye jamii zetu, pamoja na kuimarishe mtazamo imara wa siku zijazo. Dhima ya Milenia 2015 ni: kutambua na kuweka wazi majukumu muhimu la wanawake katika jamii na kuonyesha upungufu wa jamii kutotambua uwezo wa wanawake kama wajenzi wa jamii na dunia mbadala ya siku zijazo, kwa kuzingatia sifa zao, kama vile uwezo wa kupatanisha jamii, kutandaa katika ngazi zote, uwezo wa kuwa watetezi wa kijamii, kupambana na majanga na migongano ya kibinadamu kwa kujenga mshikamano kati ya wanawake.

Wanawake wote wanaoshiriki kwenye Milenia 2015, mara zote wanaonesha ushiriki wao kwa kushirikishana kazi na shughuli zao. Ni kwa njia hii wanawake wamedhihirisha kwamba kujenga nguvu za pamoja na kutandaa ni muhimu katika ngazi zote, kuanzia ngazi za kijamii, ambazo zinapambana na hatari kubwa, ngazi za kikanda, kuhusiana na mahitaji ya pamoja, na dunia kwa ujumla, kutokana na kuwepo na kukua kwa mwingiliano duniani.

Milenia 2015 , kupitia matumizi ya njia za mawasiliano ya kisasa, inatoa fursa kubwa kwa wanawake duniani kote kuwasiliana, na hivyo, kuweka wazi majukumu yao kwao wenyewe, na kwa dunia nzima. Kutandaa kunaimarishwa na kuenea kwa mawasiliano, na pia uelewa wa kina, nini wanawake wanafanya, na mchango wao katika sehemu mbalimbali duniani.

Wanawake, katika Milenia 2015, wanatoka mazingira tofauti, tamaduni tofauti na ushiriki tofauti kwenye jamii zao. Wanakutana pamoja wakiwa na lengo la kuweka wazi majukumu yao ndani ya kila jamii, na pia kujenga njia mbadala za siku zijazo, kwa kuzingatia majukumu yao tofauti, lakini yenye mwamko wa pamoja.

Ni mkakati wa kidunia, unaohusisha dunia nzima, katika kutafuta nini kinawavutia wanawake pamoja, na wakati huo huo, tofauti zao ni zipi, na kuzitumia tofauti hizo kuelekeza tofauti zao katika kushirikishana malengo yafuatayo: kutambua majukumu ya wanawake na kujenga uwezo wao kama watetezi wa jamii ambao wanaweza kuleta

mabadiliko makubwa na siyo kama wahanga tu, kama ambavyo mara nyingi inafikiriwa hivyo.

Milenia 2015 inawaonesha wanawake wenyewe na dunia, kwamba wanawake wanaweza kuleta mabadiliko na kujenga jamii shirikishi na yenye kuthamini utu.

Eleonora Barbieri Masini,

Januari 2010

*Eleonora Barbieri Masini, ni Profesa Maarufu, Kitivo cha Sayansi ya Jamii, Chuo Kikuu cha Gregorian, Rome.*

*Imetafsiriwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP)*

*Translated by Tanzania Gender Networking Programme (TGNP)*

*February 2010 [optional]*